THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2
(Kwa Watahiniwa Wahioko na Wasiokuwa Shuleni)

MUDA: Saa 2½ *Ijumaa 10 Oktoba 2008 mchana*

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne** (4), swali **moja** (1) kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

CIVIL EDUCATIONS ASSOCIATION
P. O. BOX ... CET A3

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi.

Scanned by CamScanner

SEHEMU A: QUR-AN

1. Toa mafunzo **sita (6)** yatokanayo na suratudh-Dhuha (93:1-11).

2. Salman Rushdie katika kitabu chake cha "Satanic Verses" amedai kuwa Qur-an ni aya za shetani. Kwa kurejea Qur-an yenyewe chambua udhaifu wa dai hili.

3. Andika tafsiri ya suratul-Kauthar (108:1-3) kisha chambua mafunzo yatokanayo na sura hii.

SEHEMU B: TAWHIID

4. *"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mungu na mwisho wa Mitume, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu". (33:40).*
Kwanini hapana haja ya kuja mtume mwingine baada ya mtume Muhammad (s.a.w)?

5. *"Na katika ardhi zipo (alama namna kwa namna za kuonesha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu) kwa wenye yakini. Na katika nafsi zenu (pia zimo alama nzo), Je! Hamuoni?" (51:20-21).*
Toa dalili **nane** (8) kuonesha kuwepo kwa Allah (s.w.) kutokana na nafsi ya mwanadamu.

6. Nini maana ya kuamini Qadar ya Allah (s.w.) katika mchakato wa maisha ya kila siku?

SEHEMU C: FIQH

7. Amina amefariki na kuacha wafuatao:
   (a) Mume wake
   (b) Mtoto mmoja wa kiume
   (c) Watoto wawili wa kike
   (d) Dada wawili wa kwa mama na baba

   Hakuwa na deni bali aliusia ¼ ya mali yake itolewe sadaqa kwa ajili ya kujenga shule ya Kiislamu. Kwa kuzingatia mafungu, gawa urithi kwa wahusika ukitoa maelezo kwanini kila mmoja anastahiki kupata fungu hilo.

8. Ainisha lengo la Hija kisha eleza kwa nini wengi hawafikii lengo hilo.

9. *"..... Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala Hakutakieni yaliyo mazito....."*. *(2:185).*
Kwa kuzingatia aya hii onesha namna Allah (s.w) alivyotahafifisha swala kwa **mgonjwa** na **msafiri**.

Scanned by CamScanner

SEHEMU D: TAREKH

10. Toa mafunzo **nane (8)** yatokanayo na historia ya Nabii Nuhu (a.s.) kam ilivyoainishwa katika Qur-an.

11. Ainisha mafunzo **nane (8)** yatokanayo na kuandaliwa Mtume (s.a.w) na Mola wake **kiil-hamu** na **kimafunzo.**

12. *"Bila shaka tumekwishakupa kushinda kuliko dhahiri." (48:1).*
Bainisha matukio **matano (5)** yanayodhihirisha ushindi kwa Waislamu baada ya mkataba wa Hudaybiya.

Scanned by CamScanner